

HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI

SAYANSI NA TEKNOLOJIA DARASA LA NNE, OKTOBA 2024

SEHEMU A: (Maksi 30)

1. Chagua herufi ya jibu sahihi na uandike kwenye kisanduku ulichopewa

- i. Zakaria alitaka kujua urefu wa chumba. Ni kipi kati ya vifaa vifuatavyo alikitumia?
(A) Amita (B) Kipima ujazo (C) Kipima joto (D) Tepu []
- ii. Wakati mwalimu wa sayansi kutoka shule ya msingi Likon'go akiwafundisha darasa la nne kuhusu kinga ya mwili alieleza kazi ya seli nyeupe za damu mwilini. Ni ipi kati ya zifuatazo ni kazi ya seli nyeupe za damu?
(A) Kujenga mwili (B) Kusafirisha oksijen (C) Kulinda mwili dhidi ya magonjwa
(D) Kuupa mwili nishati []
- iii. Viumbe hai wana sifa mbalimbali. Kitendo cha kiumbe hai kutoa taka mwilini kinaitwa
(A) Kujongea (B) Kukua (C) Kuzaliana (D) Utoaji takamwili []
- iv. Malaria ni ugonjwa wa kuambukiza unaosabaishwa na kimelea kinachoitwa?
(A) Anofelesi jike (B) Plasmodiam (C) Anofelesi dume (D) Mbu kyuleksi []
- v. Joto husafiri katika maada yabisi kwa njia ya
(A) Mpitisho (B) Msafara (C) Mnutudisho (D) Kipitisha mwanga []

2. Oanisha fungu A na fungu B ili kuleta maana kamili

NO	FUNGU A	MAJIBU	FUNGU B
i.	212°F	[]	A. Mmeng'enyo wa chakula huuanzia hapa
ii.	Skrini	[]	B. Hutabiri matokeo ya uchunguzi
iii.	Matege	[]	C. Kizingiti cha mgando cha maji
iv.	Iliamu	[]	D. Ufyonzaji wa chakula
v.	Dhanio	[]	E. Upungufu wa vitamini C
		[]	F. Kizingiti cha myeyuko cha maji
			G. Huonesha picha na maandishi
			H. Upungufu wa vitamini D

3. Jaza sehemu zilizo wazi kwa kutumia maneno yaliyo kwenye kisanduku

Maada Ripoti Hewa ya oksijeni maji huduma ya kwanza nishati

- i. _____ ni msaada wa haraka anaopatiwa majeruhi.
ii. Maada inayopatikana katika hali zote tatu ni _____
iii. Kitu chochote chenye uzito na kinachochukua nafasi huitwa _____
iv. _____ hutumika katika mwili kuunguza chakula na kuzalisha nishati
v. _____ huandikwa baada ya uchunguzi wa kisayansi kwa lengo la kutunza taarifa kwa matumizi ya baadae.

4. Pang'a upya hatua za kufanya uchunguzi wa kisayansi kuanzia ya kwanza hadi ya mwisho

- i. Kukusanya data []
ii. Kubuni dhanio []
iii. Kubaini tatizo []
iv. Hitimisho []
v. Kufanya jaribio []

5. Jaza nafasi zilizo wazi

- i. Vyakula vinavyojenga mwili vinaitwa _____
ii. _____ ni uwezo wa mwili kupambana dhidi ya magonjwa
iii. Taja aina mbili za majiko yanayochangia ukataji wa miti hovyo
(a) _____
(b) _____
iv. Kitendo cha kusafirisha taarifa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine kinaitwa _____

v. Ili chakula kidumu kwa muda mrefu bila kuharibika kinatakiwa kuhifadhiwa kwenye kifaa kinachoitwa
